



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA  
YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UCHAGUZI MKUU  
WA MWAKA 2025**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, na kanuni ya 22 na 23 za Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu rejewa, Tume inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia kiunganishi (*link*) <https://ams.inec.go.tz> katika Mfumo wa Kusajili Watazamaji, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari (Accreditation Management System - AMS).

Taasisi au asasi ya kiraia itakayoomba inapaswa kuwa na vigezo vifuatavyo:-

- (i) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- (ii) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- (iii) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

- (iv) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
- (v) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
- (vi) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- (ii) kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;
- (iii) kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika; na
- (iv) kujaza anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 21 Aprili, 2025 hadi 20 Mei, 2025.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

Limetolewa leo tarehe 21 Aprili, 2025 na:

Kailima, R. K  
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

